

TATHIMINI YA SABABU ZA KUFANYIKA KWA MAKOSA YA KIMATAMSHI NA KIOTHOGRAFIA KATIKA KISWAHILI: MFANO WA SHULE TEULE ZA SEKONDARI WILAYANI NYARUGENGE NCHINI RWANDA

Pascal Sebazungu

Chuo Kikuu cha Rwanda
psebazungu@gmail.com

Makala imechunguza sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika lugha Kiswahili. Tafiti nyingi zilizofanyika zilijikita zaidi katika uchanganuzi wa makosa ya kimatamshi na kiothografia yanayofanyika katika Kiswahili bila kutoa sababu zinazosababisha makosa hayo. Kutokana na hayo, utafiti wetu ulitathmini vyanzo vya kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia miongoni mwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili kama lugha yao ya pili. Makala iliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa iliyoasisiwa na Corder mnamo mwaka 1967. Sampuli ya watafitiwa ilihusisha walimu 6 wa Kiswahili na wanafunzi 15 kutoka shule teule tano tofauti. Shule hizi ziliteuliwa kwa kuwa zinakaa katika eneo lenye Waislamu wengi ambao ni wazungumzaji wakubwa wa Kiswahili. Shule hizo zilikuwa Gs. Camp Kigali, Gs. Cyahafi, Shule ya Kiufundi ya Leading, Lycée Notre Dame de Citeaux na Epä S^t Michel. Data zilikusanywa kwa kutumia mahojiano, ushuhudiaji na udurusu wa nyaraka. Matokeo ya utafiti yalibainisha kuwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili yanatokana na ujuzi finyu wa lugha lengwa, kutojua kanuni za kisarufi, ukiukaji wa kanuni za kisarufi, uhamishaji wa vipengele vya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili, wingilugha katika ujifunzaji wa Kiswahili pamoja na mtazamo hasi dhidi ya lugha ya Kiswahili.

Dhana za Msingi: Makosa ya Kimatamshi, Othografia

1.0 Utangulizi

Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya pili katika mazingira ya lugha ya kwanza ni sababu kuu ya kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia (Felician, 2019 & Zighe, 2021). Naye Alebaid (2021) katika athari za lugha ya kwanza katika ujifunzaji wa Kiingereza kama lugha ya pili, anadhihirisha kuwa lugha ya kwanza ni chanzo kikubwa cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia yanayojitokeza katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa lugha ya pili. Licha ya kuonesha lugha ya kwanza kuwa chanzo cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa lugha ya pili, utafiti huo ulifanyika kuhusu ujifunzaji wa Kiingereza ambayo si sawa na Kiswahili.

Kwa hiyo, kulihitajika kufanya utafiti wa Kiswahili kuhusu vyanzo vya kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia. Uchunguzi huo ulifanyika ili kutathimini sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia ya wanafunzi wa Kiswahili wa shule za sekondari. Pamoja na hayo, makosa hayo ya kimatamshi na kiothografia yanafanyika kutokana na kuingiliana kwa vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na semantiki (Matinde, 2012; Kanake, 2013; Obara, 2014). Kazemian na Hashemi (2014) wanadhihirisha kutojua kanuni tofauti za kisarufi ni chanzo kikubwa cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa lugha ya pili.

Makala hii inatathimini sababu za ukiukaji wa matamshi na maandishi ya lugha ya Kiswahili ikizingatia kanuni za kimatamshi na kiothografia ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wajifunzaji wa Kiswahili katika shule za upili. Zaidi ya hayo, Kemunto na wenzake (2017) na Barasa (2021) wanabainisha kuwa ukiukaji wa kanuni za kisarufi ni sababu kuu ya kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Vivyo hivyo, Butoyi (2022) anaonesha kuwa mwingiliano wa lugha nyingi katika ujifunzaji wa lugha ya pili ni chanzo kikuu cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili.

Isitoshe, Keshavarz (2006) anabainisha kuwa uhamishaji wa vipengele vya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili ni sababu kuu inayosababisha kuwapo kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika lugha lengwa. Hivyo basi, vipengele hivyo vinahamishwa kutokana na kuathiriwa pakubwa na lugha ya kwanza ya wanafunzi, wanapojifunza lugha ya pili (Mulei, 2014). Zaidi ya hayo, wanafunzi hao wanahamisha vipengele hivyo kwa kuwa hawana ujuzi wa kutosha katika lugha lengwa.

Pamoja na kuhamisha vipengele vya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili, wanafunzi wa lugha ya pili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na kufananisha vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na kisemantiki vya lugha ya kwanza na vile vya lugha ya pili (Mulama, 2016). Baada ya kupitia maandiko tofauti kuhusu sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa lugha ya pili, tulitambua kuwa tafiti hizo zina dosari mbalimbali.

Mosi, maandiko tofauti ya Mulei (2014; 2021) yanazungumzia sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi au kiothografia kivyake. Pili, maandiko hayo hayazungumzii sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia kwa pamoja. Tatu, tafiti nyingi zinazungumzia sababu za kufanyika kwa makosa hayo katika Kiingereza na Kifaransa ambazo zinatofautiana na Kiswahili kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na semantiki (Rizki na wenzake, 2024).

Kutokana na uchunguzi wa awali wa makosa ya kimatamshi na kiothografia, makala hii inachanganua sababu mahususi zinazosababisha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili. Makala hii inachanganua sababu za utokeaji wa makosa ya kimatamshi na kiothografia ili kuondokana na makosa ya kisarufi na kujenga matumizi sahihi ya Kiswahili miongoni mwa wajifunzaji wa lugha ya pili. Aidha, matokeo ya utafiti yatasaidia walimu wa Kiswahili kutambua kirahisi vyanzo vya makosa ya kimatamshi na kiothografia yanayofanyika katika ujifunzaji wa Kiswahili wilayani Nyarungenge na nchini kote kwa ujumla.

2.0 Nadharia ya Utafiti

Utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa ambayo iliasisiwa na Corder mnamo mwaka 1967. Nadharia hii inaonesha kuwa makosa yanayofanywa na wanafunzi wa lugha si jambo baya bali ni sehemu ya mchakato mzima wa kujifunza lugha. Pamoja na maelezo hayo, Corder (1967) anasisitiza kuwa makosa yanayofanyika katika ujifunzaji wa lugha ya pili, yanaweza kusaidia kuelewa jinsi wanafunzi wanavyojifunza lugha husika na kutambua maeneo wanamopata changamoto tofauti. Makala hii inazingatia mihimili ya nadharia hii katika kukusanya data, kubainisha makosa, kufafanua makosa, kuyaeleza na kuyatathmini makosa husika ya kimatamshi na kiothografia na kisha kuwasilisha matokeo ya sababu za ukiukaji wa kimatamshi na kiothografia katika mazungumzo na maandishi ya lugha ya Kiswahili miongoni mwa wajifunzaji wa Kiswahili nchini Rwanda. Mihimili hiyo ilitusaidia pakubwa kukusanya, kuwasilisha na kuchambua data za uwandani. Data hizo ziliwasilishwa na kuchanganuliwa kwa kuzihusisha na zile za upili zinazohusiana na sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa Kiswahili.

3.0 Mbinu za Utafiti

Mrengo wa kitaamuli ylitumika kwa kuchukua sampuli lengwa. Sampuli hiyo ilihusisha walimu wa Kiswahili 6 na wanafunzi 15 kutoka shule teule za upili zilizoko wilayani Nyarugenge nchini Rwanda. Shule hizo zilikuwa Gs. Camp Kigali, Gs. Cyahafi, Shule ya Kiufundi ya Leading, Lycée Notre de Citeaux na EPA St Michel. Zaidi ya hayo, data zilikusanywa kwa kutumia mahojiano, ushuhudaiji pamoja na udurusu wa nyaraka.

4.0 Sababu za Ukiukaji wa Matamshi na Othografia

Data za uwandani zilibaini sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa Kiswahili kama ifuatavyo:

4.1 Uhamishaji wa Vipengele vya Kifonolojia vya Kinyarwanda kwa Kiswahili

Data za mahojiano na walimu wa Kiswahili zilibaini kuwa wanafunzi wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na kuhamisha vipengele vya kifonolojia vya Kinyarwanda katika othografia ya Kiswahili. Hii ilithibitishwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule A kwa kusema:

Dondoo Na.01

Mimi kama mwalimu wa Kiswahili, ninaona kuwa wanafunzi wangu wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili. Makosa hayo yanatokana na kuhamisha vipengele vya kifonolojia vya Kinyarwanda katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kwa mfano, wanasema “bale batoto banacheza mpira”.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo la mtafitiwa huyu linaonesha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanafanya makosa tofauti ya kimatamshi wanapohamisha vipengele vya kifonolojia vya Kinyarwanda (L1) wakati wa kutunga sentensi za Kiswahili (L2). Makosa hayo yanatokana na mazingira ya Rwanda wanamosomea Kiswahili. Hoja hiyo ya usomaji wa lugha ya pili katika mazingira ya lugha ya kwanza inathibitishwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule B kwa kusema yafuatayo:

Dondoo Na.02

Mimi kama mwalimu wa Kiswahili, ninaona kwamba wanafunzi wetu wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa Kiswahili. Kwa hiyo, makosa hayo yanatokana na mazingira ya Kinyarwanda ambamo wanafunzi wetu wanasomea Kiswahili. Kwa mfano, wanafunzi wetu wanatoka katika familia ambazo hazikusoma. Kutokana na kutosoma huko, familia hizo zinatumia Kinyarwanda muda mwingi katika shughuli tofauti. Matumizi ya Kinyarwanda ya muda mrefu yanawaathiri wanafunzi wetu kwa kiwango kikubwa, wanapotamka na kuandika Kiswahili.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Madondoo Na. 01 na 02 yanatuonesha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanatamka na kuandika vibaya Kiswahili kutokana na kuhamisha vipengele vya lugha ya Kinyarwanda katika matamshi na othografia ya Kiswahili. Keshavarz (2006) anabainisha kuwa uhamishaji wa vipengele vya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili ni sababu kuu inayosababisha kuwepo kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika lugha lengwa. Nao Msanjila (2005) na Mwangi (2015) wanabainisha kuwa wanafunzi wa lugha ya pili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na mazingira ya lugha ya kwanza wanamojifunzia lugha ya pili. Hali hii inawasababishia wanafunzi hao kuhamisha vipengele vya kifonolojia na kimofolojia vya lugha ya kwanza katika matamshi na othografia ya lugha ya pili.

4.2 Ujuzi Finyu katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Data za mahojiano na wanafunzi zilibaini kuwa makosa ya kimatamshi na kiothografia yanatokana na ujuzi mdogo wa Kiswahili hasahasa msamiati wake kama ilivyothibitishwa na wanafunzi kutoka shule A pale waliposema yafuatayo:

Dondoo Na. 03

Sisi tunashindwa kutamka Kiswahili kwa kuwa hatuna ujuzi wa kutosha katika lugha hiyo. Zaidi ya hayo, tuna msamiati mchache katika Kiswahili. Tunapojaribu kuongea lugha ya Kiswahili, tunakosa la kusema. Tunapokosa la kusema, tunachanganya msamiati wa Kinyarwanda, Kiingereza na ule wa Kiswahili.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo la watafitiwa hao linatuarifu kuwa wanafunzi wanashindwa kutamka vizuri Kiswahili. Matamshi mabaya hayo yanatokana na ujuzi finyu pamoja na uhaba wa msamiati katika lugha ya pili. Uhaba huo wa msamiati unasababishwa na ukosefu wa mazoezi ya kutosha ya kimazungumzo ya darasani (Ngenzi, 2023). Vivyo hivyo, jambo hilo la mazoezi ya kimazungumzo hapo darasani liliungwa mkono na wanafunzi kutoka shule B pale waliposema:

Dondoo Na. 04

Sisi kama wanafunzi wa Kiswahili tunafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kwa kuwa hatuna uzoefu wa kufanya kazi za Kiswahili na kuziwasilisha darasani. Zaidi ya hayo, tunaogopa kuongea Kiswahili darasani. Pamoja na hayo, tunakosa msamiati mwafaka wakati tunapongea na kuandika Kiswahili. Isitoshe, tunafanya makosa hayo kwa kuwa tunazoea kuongea na kuandika Kinyarwanda mara nyingi. Kutokana na hayo, tunapongea na kuandika Kiswahili, kunajitokeza msamiati wa Kinyarwanda.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Madondoo Na. 03 na Na. 04 yanatuonesha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na mambo tofauti kama vile: woga, ukosefu wa msamiati mwafaka wakati wa kuongea na kuandika Kiswahili. Vilevile, makosa hayo yanafanyika pale panapojitokeza vipengele tofauti vya Kinyarwanda (L1) wakati wa kuongea na kuandika Kiswahili (L2). Ndikubwimana (2023) anasema kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanaogopa kuzungumza Kiswahili kwa kuwa hawana uzoefu wa kuongea lugha hiyo.

Naye Alebaid (2021) anabainisha kuwa lugha ya kwanza ni chanzo kikuu cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa lugha ya pili. Pamoja na hayo, Ndikubwimana (Khj) katika changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili ya wanafunzi Wanyarwanda, anabainisha kuwa wanafunzi hao wanaosoma Kiswahili kama lugha yao ya pili wanakabiliwa pakubwa na changamoto ya ukosefu wa ujuzi katika lugha ya pili. Hali hii ilithibitishwa na wanafunzi kutoka shule Ch kwa kusema yafuatayo:

Dondoo Na.05

Sisi tunashindwa kuuliza na kujibu maswali darasani kwa kuwa tunakosa msamiati wa kutumia wakati wa kutunga sentensi za Kiswahili. Pengine, hatujui nyakati za vitenzi zinazoweza kutusaidia kutunga sentensi za lugha ya pili.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo hili linabainisha kuwa wanafunzi wanakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa msamiati na ujuzi mdogo wa nyakati za vitenzi zinazotumiwa, wanapotunga sentensi. Hali hii inawasababishia kutozungumza na kuandika Kiswahili kwa usahihi. Kwa mijibu wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa hili sio kosa geni kwa wanafunzi wanaojifundisha lugha ya pili ambapo inategemewa kuwa wale wanaojifunza lugha wataanza kwa kuwa na msamiati finyu, ujenzi wa kisarufi wenye makosa na baadaye uwezo wao utaongezeka taratibu kwa kadiri ya matumizi.

4.3 Kutojua Kanuni za Kisarufi katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Data za mahojiano na walimu wa Kiswahili zilionyesha kuwa wanafunzi wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na kutojua kanuni tofauti za kisarufi. Hali hii ilithibitishwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule Ch kwa kusema:

Dondoo Na.06


Mimi kama mwalimu wa Kiswahili, ninaona kuwa wanafunzi wangu wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa Kiswahili. Wanafunzi hao wanafanya makosa hayo kwa kuwa hawajui kanuni za kisarufi.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo la mtoa taarifa huyo linaonesha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa Kiswahili kutokana na ujuzi mdogo wa kanuni za kisarufi. Ni dhahiri kwamba wanafunzi wa lugha ya pili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na kutojua kanuni za kisarufi zinazoongoza muundo wa sentensi za lugha ya pili. Kazemian na Hashemi (2014) wanabainisha kuwa

wanafunzi wa lugha ya pili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia wanapoongea na kuandika lugha lengwa.

Data za upili zinaoana na zile za ushuhudaji. Tuliposhuhudia somo la Kiswahili hapo darasani, tuliona kuwa wanafunzi wa Kiswahili kutoka shule A walishindwa kutamka na kuandika sentensi tofauti za Kiswahili kwa usahihi. Pamoja na hayo, data za uchambuzi wa nyaraka kutoka notisi tofauti za wanafunzi zilibaini kuwa wanafunzi wa Kiswahili wanafanya makosa tofauti ya kiothografia kwa kuwa hawajui kanuni za kisarufi.



Kielelezo Na. 01

Uchunguzi wa kielelezo cha notisi cha hapo juu, unaonesha kuwa wanafunzi wa Kiswahili walifanya makosa ya kiothografia ya aina saba. Mosi, wanafunzi hao walitumia herufi ndogo mwanzoni mwa sentensi walipotunga sentensi tofauti za Kiswahili. Kwa mfano, waliandika data hizo na kuzifanya kazi kuzichambua badala ya data hizo na kuzifanyia kazi wakati wa kuzichambua. Nanda na wenzake (2016) wanabainisha kuwa wanafunzi wa lugha ya pili wanatumia herufi kubwa kwa njia isiyo sahihi wanapotunga sentensi tofauti za lugha lengwa. Pili, walichanganya herufi ndogo na kubwa wakati wa kutunga sentensi mbalimbali za Kiswahili. Kwa mfano, waliandika "Uchambuzi ndiyo Unaowawezesha wanafasi Kuhakikisha Kuwa kazi fulani ni ya kifasihi au la" badala ya "uchambuzi ndio unaowawezesha wanafasihi kuhakikisha kuwa kazi fulani ni ya kifasihi au la."

Tatu, wanafunzi hao walidondosha baadhi ya sauti katika maneno tofauti ya Kiswahili, walipoyaandika maneno husika. Kwa mfano, waliandika wanafasi badala ya wanafasihi.

Mushumbwa (2022) anadhihirisha kuwa watumiaji wa Kiswahili wanadondosha baadhi ya sauti, wanapoandika maneno mbalimbali ya Kiswahili.

Nne, wanafunzi hao walichopeka sauti za Kinyarwanda katika maneno ya Kiswahili pale walipoyaandika maneno hayo. Kwa mfano, **datata** badala ya data. Bizimana (2022) anaonesha kuwa wanafunzi wa lugha ya pili wanachopeka baadhi ya sauti katika maneno ya Kiswahili wakati wa kuyaandika.

Tano, walibadilishana fonimu fonimu wakati wa kuandika vitenzi tofauti vya Kiswahili. Kwa mfano, waliandika zinazohuzu badala ya zinazohusu. Butoyi (2022) anaonesha kuwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili kama lugha yao ya pili, wanakabiliwa na changamoto kubwa ya ubadilishanaji wa fonimu, wanapoandika maneno mbalimbali ya Kiswahili.

Zaidi ya hayo, wanafunzi hao waliathiriwa pakubwa na othografia ya Kinyarwanda (L1), walipoandika vitenzi vya Kiswahili (L2). Kwa mfano, waliandika **hawuezi** badala ya kuandika hauwezi. Alebaid (2021) anabainisha kuwa wajifunzaji wa lugha ya pili wanaathiriwa pakubwa na lugha yao ya kwanza, wanapotamka na kuandika maneno tofauti ya Kiswahili.

Isitoshe, wanafunzi hao walishindwa kupatanisha nomino na kitenzi kishirikishi kipungufu, walipotunga sentensi tofauti za Kiswahili. Kwa mfano, waliandika **Uchambuzi ndiyo** Unaowawezesha wanafasi Kuhakikisha Kuwa kazi fulani ni ya kifasihi au la badala ya uchambuzi ndio unaowawezesha wanafasihi kuhakikisha kuwa kazi fulani ni ya kifasihi au la.

Hali zote hizi zilizojadiliwa zinasadifu msingi wa Nadharia ya Uchanganuzi Makosa hasa kwa wanafunzi wanaojifunza lugha ya pili. Aidha, Ntawiyanga (2019) anadhihirisha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanashindwa kupatanisha nomino, vivumishi tofauti pamoja na aina nyingine za maneno ya Kiswahili, wanapotunga sentensi mbalimbali za lugha ya pili. Kulingana na maelezo ya wanaisimu wa hapo juu, inaonekana kuwa wanafunzi wa lugha ya pili wanakabiliwa pakubwa na changamoto nyingi katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa lugha lengwa kama vile: matumizi mabaya ya herufi kubwa, ubadilishanaji wa fonimu, udondoshaji, uchopekaji pamoja na upatanishi usio sahihi wa kisarufi unaojitokeza, wanapoandika maneno tofauti ya lugha ya pili.

4.4 Ukiukaji wa Kanuni za Kisarufi

Data za mahojiano na walimu wa Kiswahili zilionesha kuwa wanafunzi wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na kukiuka kanuni za kisarufi. Hii ilithibitishwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule D kwa kusema:

Dondoo Na. 07

Kwa mtazamo wangu, ninaona kuwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili yanasababishwa na kukiuka kanuni mbalimbali za kisarufi. Ukiukaji huo unajitokeza pale wanafunzi wanapotamka na kuandika sentensi tofauti za Kiswahili. Kwa mfano, wanatamka “mbuzi yangu imekufa”. Mfano mwingine, “hii jembe inalima sana”.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo Na. 07 linabainisha kuwa wanafunzi wa Kiswahili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kwa kukiuka kanuni mbalimbali za kisarufi katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kemunto na wenzake (2017) wanabainisha kuwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili wanafanya makosa tofauti kutokana na kukiuka kanuni tofauti za kisarufi za lugha ya pili. Kauli hii ina maana kuwa wanafunzi wanaosoma Kiswahili wanafanya makosa, wanapotamka na kuandika Kiswahili kwa kuwa wanakiuka kanuni zinazoongoza utungaji wa sentensi katika lugha ya pili.

Data hizi zinawiana pakubwa na data za ushuhudiaji. Tuliposhuhudia somo la Kiswahili hapo darasani, tuliona kuwa wanafunzi wa lugha ya pili walitunga sentensi tofauti zisizo sahihi kwa ajili ya kukiuka kanuni tofauti za kisarufi. Pamoja na hayo, ukiukaji huo wa kanuni za kisarufi ulijitokeza katika uchambuzi wa mitihani, majaribio, mazoezi ya Kiswahili. Hali hii inathibitishwa na data kutoka uchambuzi wa mtihani ulifanywa na wanafunzi kutoka shule B.

2. Tumia vivumishi na vitenzi, vipatikanavyo mabanoni kwa usahihi (Alama 10)
1. Kazini (enyewe) (kupendeza).
...Kazini...penyewe...panapendeza.....
 2. Mahali (tagatifu)(kutukuzwa).
...Mahali...patagatu...patakatifu...panatukuzwa.....
 3. Shimoni (le) (kuwa na) nyoka.
...Shimoni...mle...huwa...pana...nyoka.....
 4. Shuleni (zuri)(kujulikana).
...Shuleni...nzuri...pejulikana...(panajulikana).....
 5. Ziwani (pi)(kujitokeza) mamba wakali?
...Ziwani...wapi...palitokeza...mamba...wakali...?.....

Kielelezo Na. 02

Kama inavyoonekana, mifano ya hapo juu inabainisha kuwa wanafunzi wa Kiswahili walifanya makosa ya kiothografia pale walipokiuka kanuni za kisarufi. Mosi, walishindwa kupatanisha nomino na kivumishi rejeshi katika sentensi. Kwa mfano, waliandika kazini penyewe panapendeza badala ya kazini kwenyewe kunapendeza. Pili, wanafunzi hao walishindwa kupatanisha nomino, kivumishi kiulizi na kitenzi, walipotunga sentensi tofauti za Kiswahili. Kwa mfano, ziwani wapi palijitokeza mamba wakali badala ya ziwani mupi mljitokeza mamba wakali? Tatu, wanafunzi hao walishindwa kupatanisha kivumishi kionyeshi na kitenzi katika sentensi. Kwa mfano, waliandika shimoni mle huwa pana nyoka badala ya shimoni mle mna nyoka. Ntawiyanga (2015) anaonesha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanatatizika pale wanapopatanisha nomino, kivumishi kionyeshi, kivumishi kimilikishi, kiulizi, kivumishi cha idadi, kivumishi cha sifa pamoja na aina nyingine za maneno ya Kiswahili. Kutokana na maelezo ya mtaalamu huyu, inadhihirika kuwa wanafunzi wa lugha ya pili wanafanya makosa tofauti ya kiothografia kutokana na kukiuka kanuni za kisarufi zinazoongoza utungaji wa sentensi ya lugha ya pili.

4.5 Wingi Lugha katika Ujifunzaji wa Kiswahili

Butoyi (2022) anabainisha kuwa mwingiliano wa lugha nyingi katika ujifunzaji wa lugha ya pili ni chanzo kikuu cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika lugha lengwa. Kuingiliana huko kunawafanya wanafunzi watamke na waandike lugha ya pili kwa kupachika

msamiati wa lugha hizo. Kupachikwa huko kwa msamiati wa lugha hizo katika matamshi na othografia ya lugha ya pili kunatokana na kuathiriwa pakubwa na lugha hizo.

Pamoja na maelezo hayo, wingi lugha katika ujifunzaji wa Kiswahili ni chanzo kikuu cha kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia kama inavyodhihirishwa na Niyomugabo (2016) kwa kusema:

Dondoo Na.08

Wanafunzi Wanyarwanda wanafanya makosa ya kiothografia kutokana na kuchanganya Kiswahili, Kinyarwanda, Kifaransa na Kiingereza. Kwa mfano, wanaandika ninaenda ku market devant.

Chanzo: Niyomugabo (2016)

Dondoo hili linaonesha kuwa wanafunzi Wanyarwanda wanachanganya Kiswahili, Kinyarwanda, Kiingereza na Kifaransa, wanapoandika lugha ya pili. Hali inaathiri ujifunzaji wa lugha ya pili, kwa kuwa wanafunzi wanajikita kuchanganya vipengele vya kifonolojia na kimofojia vya lugha tofauti katika matumizi ya lugha ya pili. Hii inaathiri mawasiliano ya kimazungunmzo na kimaandishi kwa kuwa wanafunzi wanashindwa kuwasilisha kwa usahihi ujumbe wao katika lugha ya pili. Jambo hilo lilithibitishwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule Ch kwa kusema:

Dondoo Na.09

Kwa maoni yangu ninaona kuwa wanafunzi wetu wanafanya makosa tofauti, wanapotamka na kuandika Kiswahili. Makosa hayo yanafanyika kwa kuwa wanafunzi wetu wanatoka katika familia zinazooonea lugha tofauti kama vile: Kiingereza, Kiarabu kwa Waislamu pamoja na Kifaransa. Zaidi ya hayo, wanafunzi hao wanaosoma mchepuo wa utalii, wanasoma lugha za Kiingereza, Kifaransa pamoja na Kinyarwanda. Ujifunzaji wa lugha hizo unaathiri pakubwa matamshi na othografia ya Kiswahili. Kwa mfano, wanapoandika na kuwasilisha kazi za Kiswahili wanapachika msamiati wa Kiingereza na Kifaransa. Hii inawasabishia kutowasilisha kwa usahihi ujumbe wao mbele ya wenzao.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo la mtafitiwa huyu linadhihirisha kuwa wanafunzi wa Kiswahili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na kuchanganya msamiati wa Kifaransa, Kiarabu na Kiingereza, wanapotamka na kuandika Kiswahili. Hali hii inaathiri mawasiliano ya kimazungumzo na kimaandishi, kwa kuwa wasikilizaji na wasomaji wao wanashindwa kuelewa ujumbe unaokusudiwa kutolewa. Blommaert (2010) anabainisha kuwa mchanganyiko wa lugha unaathiri mawasiliano ya kimazungumzo kutokana na kuingiliana kwa mila na desturi za watu kutoka mataifa tofauti.

4.6 Mtazamo Hasi Dhidi ya Kiswahili

Data za mahojiano na walimu wa Kiswahili zilibainisha kuwa wanafunzi wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na mtazamo hasi wanaomiliki dhidi ya Kiswahili. Hii ilithibitishwa na mwalimu wa Kiswahili kutoka shule B kwa kusema:

Dondoo Na. 10:

Kwa mtazamo wangu kama mwalimu wa Kiswahili, ninadhani kuwa wanafunzi wetu wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili kutokana na maoni potofu dhidi ya Kiswahili. Zamani za kale nchini Rwanda watu walikuwa wakisema kuwa Kiswahili ni lugha ya wadanganyifu na majambazi. Mpaka sasa, kuna wazazi ambao wanangalikuwa na maoni potofu hayo. Mara nyingi, wazazi hao huwaambia watoto wao kuwa Kiswahili hakina hadhi sawa ni Kiingereza pamoja na Kifaransa. Kutokana na hilo, wanawahimiza watoto wao kusoma Kiingereza na Kifaransa ambazo ni lugha zinazotumiwa katika ngazi tofauti za Serikali ya Rwanda.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Dondoo la mtafitiwa huyu linabainisha kwamba wanafunzi wa Kiswahili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kutokana na maoni potofu dhidi ya lugha hiyo ambayo yalikuwa yanajitokeza miaka kadhaa nchini Rwanda. Data hizo za uwandani zinaoanishwa na zile za upili kutoka kazi tofauti za kiutafiti kwa kujiegemeza kwa wanaisimu tofauti kama ifuatayo: mosi,

Ntahonkiriye (1996) anadhihirisha kwamba Wamishenari wa Kikatoliki walitenga na kupinga Kiswahili miaka kadhaa nchini Rwanda. Wamishenari hao walikuwa hawataki kuenea kwa Kiswahili kwa ajili ya kutosambaza dini ya Kiislamu nchini kote.

Dini hiyo ilikuwa ikitumia lugha ya Kiswahili katika shughuli zake (Ntahonkiriye, Khj). Pili, Ngenzi (2023) naye anaunga mkono hoja hiyo pale anapoonesha kuwa wanafunzi Wahehe nao hawapendi kujifunza lugha ya Kiswahili kwa kuwa wanaamini kuwa Kiswahili ni lugha ya wanamjini ambao ni Waswahili. Jambo hilo la kutopenda kujifunza Kiswahili liliungwa mkono na mwalimu wa pili wa Kiswahili kutoka shule teule ya pili. Mwalimu huyo alisema:

Dondoo Na.11

Mimi kama mwalimu wa Kiswahili ninaona kuwa wanafunzi wetu hawana motisha, wanapojifunza Kiswahili. Hilo linatokana na kuwa Kiswahili hakipewi hadhi sawa na Kiingereza pamoja na Kifaransa katika midahalo ya kilugha. Kwa mfano, tunaona tu mashindano ya Kiingereza na Kifaransa; hatujaona hata kamwe mashindano ya midahalo ya Kiswahili yanayokutanisha shule mbili ama tatu. Kutokana na jambo hilo la kutopewa kipa umbele kwa Kiswahili katika midahalo, wanafunzi wetu wanasoma Kiswahili kwa kukipuuza.

Chanzo: Data za Uwandani (2024)

Madondoo ya walimu hao yanatuarifu kuwa wanafunzi wa Kiswahili wanafanya makosa ya kimatamshi na kiothografia kwa kuwa hawana motisha wakati wanaposoma Kiswahili. Ukosefu huo wa motisha unasababishwa na uhaba wa mashindano ya Kiswahili katika shule tofauti za upili. Kutokana na hayo, wanafunzi hao wanasoma Kiswahili kwa kukipuuza pakubwa. Upuuzaji huo unajikita mizizi katika historia ya Kiswahili nchini Rwanda (Ntahonkiriye, Khj).

Zaidi ya hayo, upuuzaji wenyewe unatokana na maoni potofu dhidi ya Kiswahili ya baadhi ya wazazi ambao wanadhani kuwa Kiswahili hakina hadhi sawa na lugha rasmi nyingine zinazotumiwa nchini Rwanda. Isitoshe, upuuzaji wa Kiswahili unasababishwa na ukosefu wa motisha wakati wa kujifunza lugha hiyo (Ndagijimana, 2013 & Wanyenya, 2020).

Kutokana na upuuzaji huo, wanafunzi Wanyarwanda wanaosoma Kiswahili wanashindwa kutamka na kuandika lugha hiyo ipasavyo kwa kuwa wanatamka na kuandika Kiswahili kama vile wanavyotamka na kuandika Kinyarwanda (Niyomugabo, 2016). Maelezo ya wataalamu hao yanatupa picha kamili kuhusu vyanzo mbalimbali vya kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika mchakato mzima wa ujifunzaji wa Kiswahili.

5.0 Mapendekezo

Kutokana na matokeo ya utafiti, makala hii inapendekeza ngazi tofauti za elimu kama ifuatavyo:

Mosi, walimu wa Kiswahili wanapaswa kufundisha lugha lengwa kwa kutumia mbinu ya ufundishaji wa lugha ya moja kwa moja. Mbinu hiyo itasaidia pakubwa kuondokana na kuhamisha kimatamshi na kiothografia vipengele vya kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia na vile vya kisemantiki vya lugha ya kwanza kwa lugha ya pili. Pamoja na hayo, mbinu yenyewe itasaidia kuondokana na mchanganyiko wa lugha tofauti katika kujifunza lugha lengwa. Pili, walimu hao wanapaswa kufundisha kanuni za kisarufi kwa kuepukana na kutojua kanuni husika zitumiwazo wakati wa kutamka na kuandika Kiswahili.

Tatu, viongozi wa shule nao wanapaswa kudhibiti ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili ili kuchunguza changamoto zinazokabili ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili. Zaidi ya kudhibiti ufundishaji na ujifunzaji huo, viongozi hao wanapaswa kununua vifaa vya ufundishaji. Ununuzi wenyewe utasaidia pakubwa kuondokana na sababu zinazowasababishia wanafunzi kufanya makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa lugha lengwa. Vivyo hivyo, Bodi ya Kitaifa inayohusika na Elimu ya Msingi inapaswa kuandaa na kutoa zana za ujifunzaji. Zaidi ya kutoa zana hizo, taasisi hiyo ya kielimu inapaswa kutoa mafunzo endelevu kwa walimu wa Kiswahili kuhusu ufundishaji wa lugha ya pili. Aidha, Bodi ya Mitihani na Udhibiti wa Shule nayo inapaswa kutahini lugha ya Kiswahili katika mitihani ya kidato cha tatu katika shule za upili pamoja na michepuoni inayofundisha Kiswahili kama lugha ya hiari.

Nne, bodi yenyewe inapaswa kukagua kwa njia endelevu ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika shule za sekondari nchini kote. Utahini na Udhibiti hivyo vitasaidia pakubwa kuondokana na sababu za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa

Kiswahili. Wizara ya Elimu nchini Rwanda nayo inapaswa kutunga na kuweka sera ya kilugha kuhusu ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili katika viwango vyote vya shule kutoka shule za chekechea, msingi, sekondari, vyuo vikuu na hata katika michepuo yote inayofundisha masomo mengine.

6.0 Hitimisho

Makala hii imejadili sababu mbalimbali za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika ujifunzaji wa Kiswahili. Kazi hii imeongozwa na Nadharia ya Uchanganuzi Makosa. Nadharia hii imetusaidia kukusanya, kuwasilisha na kuchambua data. Pamoja na hayo, imedhihirika kuwa kuna sababu nyingi za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia kama vile: ujuzi finyu katika lugha ya pili, kutojua kanuni za kisarufi, kukiuka kanuni za kisarufi, uhamishaji wa vipengele vya kifonolojia vya Kinyarwanda kwa Kiswahili, wingi lugha katika ujifunzaji wa Kiswahili na mtazamo hasi dhidi ya Kiswahili. Kutokana na sababu zinazosababisha makosa hayo, wito unatolewa kwa watafiti na wadau wa Kiswahili kuendeleza kazi zao za kiutafiti. Maendeleo ya kazi husika yataboresha ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili. Maboresho hayo yatasaidia kuondokana na sababu hizo za kufanyika kwa makosa ya kimatamshi na kiothografia katika Kiswahili.

Marejeleo

Alebaid, M. Y. (2021). Effects of First Language on the Learning of English as A Second Language. *Multi-Knowledge Electronic Comprehensive Journal for Education* 10(44), 1-16.

Arnaud, H. et Jérôme, P. (2017). *La Faute de l'Orthographe*. Paris: Editions Textuel.

Barasa, W. E. (2021). *Uhakiki wa makosa katika maandishi ya wanafunzi wa shule za upili na vitabu vya kiada wanavyotumiwa shuleni* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Moi, haijachapishwa).

Bizimana, J. (2022). *Athari za kimofolojia za lugha ya Kirundi katika ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili kwa wanafunzi wa jamii lugha ya Kirundi* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, haijachapishwa).

- Blommaert, J. (2010). *The Sociolinguistics of Globalization*. Cambridge: Cambridge University Press.
- Butoyi, D. (2022). *Tathmini ya makosa ya kisarufi ya wanafunzi wa Kingwana wanaojifunza Kiswahili Sanifu: Uchunguzi kifani wa vyuo vikuu vya Burundi* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, haijachapishwa).
- Corder, S. P. (1967). The Significance of Learners' Errors. *International Review of Applied Linguistics in Language Teaching. Scientific Research Publishing* 5, 161-170.
- Felician, F. (2019). *Makosa ya kifonolojia yanayofanywa na wazungumzaji wa Kihaya wanaojifunza Kiswahili sanifu: Mfano kutoka Bukoba Manispaa* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, haijachapishwa).
- Kanake, J. K. (2013). *Makosa ya kifonolojia miongoni mwa wanafunzi wa Kiigembe katika ujifunzaji wa Kiswahili* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, haijachapishwa).
- Kazemian, B. & Hashemi, S. (2014). A Contrastive Linguistic Analysis of Inflectional Bound Morphemes of English Azerbaijani Persian Languages: A Comparative Study. *Journal of Education and Human Development* 3(1), 593-614.
- Kemunto, A. B. na Wenzake. (2017). Makosa ya Kisemantiki katika Mawasiliano Andishi ya Kiswahili ya Wanafunzi wa Shule za Upili Nchini Kenya. *International Journal of Arts and Education* 1(2), 13-24.
- Keshavarz, M. D. (2006). *Contrastive Analysis and Error Analysis* (6th Ed.). Tehran: Rahnama Press.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha, Isimu na Nadharia: Kwa Sekondari, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers Ltd.

- Msanjila, Y. P. (2005). Problems of Writing in Kiswahili: A Case Study of Kigurunyembe and Morogoro Secondary Schools in Tanzania. *Nordic Journal of African Studies* 14(1), 15-25.
- Mulama, H. S. (2016). *Difficultés Liées à la Prononciation du Français au Kenya: Le Cas des Apprenants des Ecoles Secondaires des Comtés de Nairobi et Bungoma*. Thèse du Doctorat (Non Publiée). Université de Kenyatta.
- Mulei, M. (2014). *Uchambuzi wa Makosa ya Kimatamshi na Kiothografia katika Ujifunzaji wa Kiswahili*. Nairobi: East African Publishers.
- Mulei, A., & Amukobwa, E. (2021). The influence of first language on second language pronunciation: A Kiswahili perspective. *African Journal of Linguistics*, 41(1), 50–68.
- Mushumbwa, A. R. (2022). Makosa ya lugha katika vyombo vya habari nchini Tanzania: Uchunguzi wa televisheni. *Nuru ya Kiswahili*, 1(2), 135–163.
- Mwangi, K. J. (2015). *Makosa ya kimofo sintaksia katika lugha ya kimaongezi dhidi ya kanuni za lugha ya Kiswahili sanifu* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, haijachapishwa).
- Nanda, R. P., Inyah, N. & Gani, S. A. (2016). Students Writing Errors in an EFL Classroom. *Proceedings of the First Reciprocal Graduate Research Symposium between University of Pendidikan Sultan Idris and Syiah Kuala University*, pp. 229-236.
- Ndagijimana, J. B. (2013). *Les Facteurs de la Faible Motivation et leurs Effets sur l'Apprentissage: Cas Des Elèves de l'Ecole Normale Primaire (ENP/TTC) au Rwanda*. Thèse du Doctorat (Non Publiée). Université de Bouaké.
- Ndikubwimana, F. (2023). *Changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa Kiswahili kama lugha ya pili katika shule za upili za Rwanda: Mfano wa shule teule wilayani Musanze* (Tasnifu ya Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu, Chuo Kikuu cha Rwanda Ndaki ya Elimu, haijachapishwa).

- Ngenzi, M. (2023). *Athari za kifonolojia ya lugha ya kwanza katika mawasiliano ya wajifunzaji wa Kiswahili sanifu kama lugha ya pili: Uchunguzi kifani Kihehe* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu, Chuo Kikuu cha Dodoma, haijachapishwa).
- Niyomugabo, C. (2016). Ufundishaji wa Kiswahili katika Shule za Rwanda: Historia Tathmini ya Makosa, Matatizo na Mahitaji. *KISWAHILI* 79(3), 79-92.
- Ntahonkiriye, M. (1996). *Statut et Fonctions des Langues au Burundi*. Laval: Université Laval.
- Ntawiyanga, S. (2015). *Changamoto za kimfosintaksia miongoni mwa wanafunzi wa Kiswahili wa shule za upili wilayani Muhanga, Rwanda* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, haijachapishwa).
- Ntawiyanga, S. (2019). Makosa ya Upatanishi wa Kisarufi katika Ujifunzaji wa Lugha ya Pili: Mfano wa Wanafunzi wa Kiswahili katika Shule za Upili Wilayani Muhanga Nchini Rwanda. *Kioo cha Lugha* 17, 15-32.
- Obara, J. M. (2014). *Uchanganuzi wa makosa yanayofanywa na wanafunzi wazungumzaji wa lugha ya Ekegusii* (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi, haijachapishwa).
- Rizki, J., Gani, S.A. & Marhaban, S. (2024). Pronunciation Errors in Speaking Committed by Non-Majoring English Students: Causes and Solution English Franca. *Academic Journal of English Language and Education*, 8(1), 179-190.
- Wanyenya, W. (2020). Visababishi vya Idadi Kubwa ya Wanafunzi wa Shule za Sekondari Nchini Uganda Kutochukua Somo la Kiswahili. *East African Journal Of Swahili Studies* 2(2), 1-10.
- Zighe, M. (2021). Makosa ya kisarufi yanayofanywa na wanafunzi Wataita wa shule za msingi wanaojifunza Kiswahili sanifu katika Kaunti ya Taita Taveta nchini Kenya (Tasnifu ya Shahada ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, haijachapishwa).